BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Tano – Tarehe 20 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

21. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Je, kwa kiasi gani Zanzibar imenufaika baada ya kero 11 za Muungano kupatiwa ufumbuzi.

## Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

72. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Madawa ya kulevya ni hatari na yanapunguza nguvu kazi kwa vijana ambao ndio tegemeo letu kubwa la kuiendeleza nchi yetu. Pamoja na kuenea kwa tatizo hili katika maeneo mbali mbali nchini, jimbo la Paje nalo limekuwa na tatizo kubwa la madawa ya kulevya.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Je, ni mikakati ipi inayochukuliwa na Serikali katika kulitatua tatizo hilo.

## Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

127. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kutokana na kukuwa kwa sekta ya utalii na uwekezaji, Zanzibar inahitaji kuwa na ukumbi wa kisasa wa mikutano ya kitaifa na kimataifa.

Je, ni lini wazo la kuwa na kumbi kubwa za mikutano ya kimataifa litakamilika ili kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

6. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Serikali ilitoa Muongozo kwa Taasisi zake kufungua hesabu za benki (accounts) katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

(a) Je, hadi hivi sasa ni kwa kiasi gani Taasisi za SMZ na SMT zimefungua hesabu zao katika Benki ya Watu wa Zanzibar.

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Taasisi ambazo hazijafungua hesabu zao katika Benki hiyo kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Muongozo huo.

8. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali imekuwa na kawaida ya kufanya tathmini ya mchango wa Mashirika ya Umma kwa taifa.

Je, kwa kiasi gani Mashirika ya Umma yanachangia pato la taifa.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

100. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuandaa utaratibu wa kuwa na viwanja vya michezo vya kisasa kwa kila Wilaya.

Ni yepi matarajio ya Wizara yako katika kuitangaza Zanzibar kwenye ulimwengu wa soka kupitia utaratibu huo.

129. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kuwa na maabara ya lugha ya Kiswahili yenye vifaa vya kupima matamshi na lafdhi, kutasaidia sana kuimarika zaidi na kukuwa kwa lugha adhimu ya Kiswahili.

Je, Wizara haioni kwamba wakati umefika wa kujenga maabara ya lugha ya Kiswahili, ili kuchochea ajira nyingi za tafasiri na ukalimani.

<u>Wizara ya Afya:</u>

41. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko kuhusiana na wahitimu wa udaktari wa hapa Zanzibar au wanarudi Zanzibar kutoka nje ya nchi kwamba wanalazimishwa kwenda kufanya mafunzo kazini (internship) Tanzania bara, jambo ambalo linawawia ugumu hasa ukitilia maanani wahitimu hao hukusudia kufanya kazi Zanzibar.

(a) Je, ni upi utaratibu wa wahitimu wa fani za udaktari kutoka Zanzibar wa kufanya ‘internship’.

(b) Je, ni mabadiliko gani ya utaratibu wa kufanya ‘internship’ katika hospitali za Serikali hapa Zanzibar baada ya kubinafsishwa uendeshaji wake.

(c) Je, ni ipi takwimu ya miaka mitano iliyopita (2018/2019 - 2022/23) katika suala hili.

69. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa miaka mingi sasa wananchi wanaoihitaji huduma ya ‘Ultrasound na Full Blood Picture’ waliopo Konde na vitongoji vyake, hususan wanawake, wanaifuata huduma hiyo katika hospitali ya Wilaya ya Micheweni au Kituo cha Afya chaTumbe, ambapo ni mbali sana.

(a) Je, ni lini huduma hizi za mama na mtoto zinazojumuisha ‘Full Blood Picture’ na ‘Ultrasound’ zitapatikana katika Kituo cha Afya cha Konde ili wananchi wa Konde na vitongoji vyake, waweze kunufaika na huduma hizo.

(b) Kwa kuwa Wizara yako iliahidi kuzipeleka mashine za ‘hauntology analyzer’ na ‘Ultrasound’ katika jimbo la Konde tokea mwezi wa Septemba, 2023, Je, ni lini Wizara imezipeleka mashine hizo na katika vituo vipi vya afya katika jimbo hilo.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

144. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Sekta ya Utalii ni msingi muhimu sana kwa uchumi wa Zanzibar. Idadi kubwa ya watalii kutoka pande mbali mbali duniani kuvutiwa kuvitembelea visiwa vyetu kila mwaka inaonesha umuhimu wa sekta hii katika kuongeza mapato na maendeleo kwa nchi yetu. Hata hivyo, kuna changamoto ambazo wadau wa sekta hii wanakabiliana nazo hasa katika suala la utozaji wa kodi.

(a) Je, ni misamaha ipi ya kodi iliyotolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuongeza uwekezaji na ushindani wa Zanzibar katika soko la kimataifa la utalii.

(b) Je, ni kodi zipi ambazo Kamisheni ya Utalii imepewa ruhusa kisheria kukusanya katika sekta ya utalii Zanzibar, ili kuhakikisha utaratibu na uwiano katika makusanyo ya kodi hizo.

(b) Je, kwa wadau wa utalii wa ndani wanaomiliki gari za kibinafsi (private hire), ni aina gani za kodi wanatakiwa kulipa kwa mwaka kulingana na sheria za nchi yetu.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

53. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imejitahidi katika ukarabati na ujenzi wa madarasa mapya ya kusomea katika skuli mbalimbali za Unguja na Pemba. Hata hivyo, kuna ushahidi kwamba, baadhi ya ujenzi wa madarasa haujazingatia viwango vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vikiwemo vigezo vya mita za mraba.

(a) Je, ni vipi viwango pendekezwa vya mita za mraba kwa kila darasa kwa skuli za Serikali na kwa skuli binafsi.

(b) Kwa vile kuna utafauti mkubwa wa viwango vilivyotumika kujenga madarasa katika skuli nyingi za Serikali, ni upi muongozo kwa madarasa yasiyotimiza viwango na kwa ujenzi wa madarasa ya baadae.

(c) Je, ni ipi dhima ya Wakandarasi na Washauri Elekezi kwa madarasa yaliyojengwa chini ya viwango vilivyoelekezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>

11. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa utendaji wa Kampuni ya Uvuvi ya ZAFICO unaonekana kusuasua hadi leo hii, na kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara kadhaa kupitia Ripoti zake amekuwa akitoa hoja kwa Taasisi wanachama kuhusiana na kujiingiza kwenye mradi usio na tija.

Je, Serikali imefanya tathmini juu ya ufanisi wa Kampuni hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

55. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Wananchi wengi wamekuwa wakilithamini sana zao la maparachichi na kulichukulia kama tunda la kigeni. Hata hivyo, kuna ushahidi kwamba zao hili linaweza kunawiri Zanzibar katika maeneo mbalimbali na kuleta tija, ikiwemo ya kiuchumi.

    (a) Je, Serikali ina takwimu ipi kuhusiana na zao la parachichi na uingiaji wake Zanzibar.

    (b) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wowote kuhusiana na mahitaji ya kimazingira kwa kilimo cha maparachichi Zanzibar.

    (c) Ili zao la parachichi liweze kuwa zao lenye tija ya kiuchumi na kiafya Zanzibar, ni matayarisho yepi kwa upande wa Serikali na kwa upande wa wakulima watarajiwa wa maparachichi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

105. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    (a) Nini hasa chanzo kikuu cha migogoro ya ardhi hapa nchini mwetu.

    (b) Je, Wizara yako ina mikakati gani ya ziada ya kuliondoa tatizo hili sugu la migogoro ya ardhi nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

3. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

    Kwa kuwa kanuni za amri ya viwango vya mwendo (speed) vya kitaifa kwa barabara zote za Zanzibar tayari zimeshatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali tangu mwezi Aprili, 2023.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuweka alama za barabarani kwa uharaka kwa kuwa utekelezaji wa kanuni hizo umekuwa na changamoto kwa kutokuwepo kwa alama zinazoonesha viwango vya mwendo.

(b) Je, ni lini Jeshi la Polisi watapatiwa vifaa vya kutosha vya kupima mwendo kwa vyombo vya moto vya usafiri.

118. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoifanya tarehe 28/07/2022 katika shehia ya Mwambe na kuweka jiwe la msingi katika skuli ya Mwambe, wananchi wa Mwambe walimuomba Mheshimiwa Rais kuwajengea barabara yao kutoka Kwareni Mwambe mpaka Chanjaani skuli na Mhe. Rais alikubali ombi hilo.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Ni lini ahadi hii itatekelezwa.

**III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>**

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:</u>**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**20 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**